

# Chekechea

## ndani ya Kansas

KIJITABU CHA FAMILIA ZENYE WATOTO WACHANGA WENYE UMRI KATI YA MIAKA 3 HADI 7

KANSAS STATE DEPARTMENT OF EDUCATION

*Kansas anaongoza ulimwengu katika mafanikio ya kila mwanafunzi.*

Iliyorekebishwa Oktoba 2025

Bodi ya maono ya Elimu ya Jimbo la Kansas huweka maono yetu ya Kansans katika elimu: Kansas huongoza ulimwengu katika ufaulu wa kila mwanafunzi. Maono haya ya elimu yanahitaji mfumo unaomlenga mtoto na kutoa msaada na rasilimali kwa mafanikio ya mtu binafsi na itahitaji kila mtu kufanya kazi kwa pamoja kuyafanya maono yaazimike. Utayari wa chekechea ni moja ya matokeo matano yanayoweza kupimika ambayo yataisongeza Kansas kuelekea kwenye mawazo haya kwa sababu uzoefu wa mapema utotoni unaweka msingi wa mafanikio ya baadaye ya mtoto kitaaluma. Asante kwa jukumu muhimu ambalo tayari umechukua katika kujifunza na kukua pamoja na mtoto wako.

Kwa kutambua Shirika la W.K. Kellogg kwa msaada wake katika ufadhili wa asili wa mradi huu.

Idara ya Elimu ya Jimbo la Kansas haibagui kwa msingi wa jamii, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, ulemavu, au umri katika mipango na shughuli zake na hutoa ufikiaji sawa kwa Skauti wavulana na vikundi vinginevyo vya vijana vilivyoteuliwa. Mtu afuatae ameteuliwa kushughulikia maswali yanayohusu sera zisizo za ubaguzi: Wakili Mkuu wa KSDE, Ofisi ya Wakili Mkuu, KSDE, Jengo la Ofisi ya Jimbo la Landon, 900 SW Jackson, Suite 102, Topeka, KS 66612, (785) 296-3201.

This publication was made possible by grant number 90TP0078. Its contents are solely the responsibility of the authors and do not necessarily represent the official view of the United States Department of Health and Human Services, Administration of Children and Families.

# **Mwaka wa Chekechea:** Kugeuza Utayari wa Shule kuwa Mafanikio ya Shule

Kituo cha Rasilimali za Habari cha Mzazi wa Kansas

Idara ya Elimu ya Jimbo la Kansas



Picha kwa hisani ya: Shule za Umma za Topeka USD 501

# Ndugu wapendwa,

## Hongera! Mtoto wako hivi karibuni ataingia chekechea – ni wakati wa kufurahiwa kwa familia yako!

Kijitabu hiki kinatoa taarifa juu ya mada muhimu zifuatazo, ambazo zinaweza kumsaidia mtoto wako kujiandaa kuingia chekechea:


- Utayari wa Chekechea ni nini? 7
- Taarifa ya Kiingilio cha Chekechea 9
  - Je! Watoto wanatakiwa kwenda chekechea? 9
  - Je! Mahitaji ya mahudhurio ya chekechea ni yapi? 9
  - Je! Ni mahitaji gani ya umri wa kujiandikisha chekechea? 9
  - Je! Ni nyaraka gani zinazohitajika katika kujiandikisha chekechea? 10
- Mpito wa Chekechea 13
  - Dodoso la Umri & Hatua ® (ASQ-3 na ASQ: SE-2) 13
- Viwango Vya Kansas Vya Kujifunza Mapema 15
- Maswali ya nyongeza ambayo unaweza kuwa nayo 19
- Orodha ya Kuingia Chekechea 21
- Rasilimali 23


Wilaya ya shule yako inaweza kutoa taarifa zaidi kuhusu uzoefu maalum wa chekechea wa mtoto wako. Kujenga uhusiano na mwalimu wa mtoto wako na shule kunaweza kusaidia kuimarisha uzoefu na mafanikio ya mtoto wako.

Ikiwa unahitaji msaada wa ziada, kama vile kutafuta wilaya yako ya shule, kujifunza zaidi juu ya mahitaji ya serikali au ungependa rasilimali za ziada za kushirikisha familia, tafadhali wasiliana nasi:

1-800-WATOTO
Linapokuja suala la kumlea mtoto wako, hakuna swali linalopita mipaka. Pata usaidizi wa uzazi bila hukumu 24/7 kwa Kiingereza na Kihispania na pia lugha zingine nyingi.

- Piga simu 1-800-332-6378
- Pakua app ya simu "1800CHILDRENKS"
- Kutuma barua pepe au kutuma ujumbe mfupi 1800CHILDREN@kcsl.org
- Kutembelea 1800CHILDRENKS.org

Kituo Cha Rasilimali Za Taarifa cha Mzazi wa Kansas
www.ksdetasn.org/kpirc
(866) 711-6711

Idara Ya Elimu Ya Jimbo la Kansas
www.ksde.gov
(785) 296-3201




Walimu wa chekechea huko Kansas wamefurahi na wamejiandaa kumsaidia mtoto wako kuelekea kufaulu shuleni.

# Utayari wa Chekechea ni nini?

**Utayari wa chekechea** huanza wakati wa kuzaliwa na unatokea katika miaka ya mwanzo kabisa ya mtoto. Wewe, kama mzazi (mtu ambaye ni mlezi anaweza kuwa mzazi mwenyewe au sio mzazi wa kibaolojia), wewe ndiye mwalimu wa kwanza wa mtoto. Kila mazingira unayounda ni mazingira ya kujifunzia. Masomo na uzoefu unaompa mtoto wako huathiri namna ya kujifunza katika maisha yake yote. Utayari wa shule ni matokeo ya miaka ya mapema ya kujifunza.

> *"Utayari wa shule unahusisha zaidi ya mtoto binafsi. Utayari wa shule, kwa maana pana zaidi, ni kuhusu watoto, familia, mazingira ya mapema, shule na jamii. Watoto hawako tayari kiasili au hawako tayari kuwa shuleni. Ujuzi na maendeleo yao yanaathiriwa sana na familia zao na kupitia maingiliano yao na watu wengine na mazingira kabla ya kuja shuleni."*
>
> — Chanzo: Maxwell, K., & R.M. Clifford. 2004. Utafiti katika Mapitio: Tathmini ya Utayari wa Shule. Watoto wadogo 59 (1): 42-46.




Msingi muhimu kwa mafanikio ya baadaye na ufaulu wa kitaaluma ni utayari wa shule. Miaka kabla ya chekechea huathiri mafanikio ya baadaye. Kumpa mtoto wako lishe bora, mazoezi ya mwili na mapenzi, pia kuzungumza nao kwa kadiri inavyowezekana, husaidia kuhakikisha mtoto wako ana ujuzi wa kumsaidia kufaulu.


38°28'45"N 100°27'41W
MARS
EARTH
URANUS
NEPTUNE

# Taarifa ya Kiingilio cha Chekechea

## Je! Watoto wanatakiwa kwenda chekechea?

Sheria ya Kansas hailazimishi watoto wahudhurie chekechea. Ila, watoto wengi wa Kansas huhudhuria chekechea wanapofikia umri stahiki. Uamuzi wa kumpeleka (au kutompeleka) mtoto chekechea hufanywa na wazazi.

> *"Familia wakati mwingine hufikiria kuchelewesha uandikishaji wa mtoto ambaye ana siku ya kuzaliwa ya karibu na tarehe ya mwisho au kwa sababu wanafikiria mtoto anahitaji muda zaidi wa kukomaa.*
>
> *Utafiti unaonyesha kuwa kuchelewesha chekechea hakuleti utofauti mkubwa katika ustadi wa masomo ndani ya miaka kadhaa ya kwanza ya shule. Pia, kutoa muda zaidi huenda isiwe sababu ya kusababisha utayari zaidi bila kuweka hatua za kushughulikia wasiwasi wa ukuaji.*
>
> *Utafiti pia umeonyesha kuwa watoto walio wakubwa kuliko wenzao wanaweza kuwa na hatari kubwa ya kuwa na changamoto za kijamii au kitabia kipindi cha ujana."*
>
> — Chanzo: Kliniki ya Mayo 2019

Si kazi ya mtoto kuwa tayari kwa shule ya chekechea, ila ni jukumu la mfumo kuwa tayari kumpokea na kumshugulikia kila mtoto katika njia inayokusudiwa na inayofaa.

## Je! Mahitaji ya mahudhurio ya chekechea ni yapi?

Mara tu mtoto wako aingiapo chekechea, mahudhurio ya kawaida yanahitajika. Sheria ya Kansas KSA 72-3120 hufanya wazazi kuwajibika kwa kuhitaji mtoto ambaye amefikia umri wa miaka 7 na ambaye wanawajibikia kuhudhuria shule kila wakati hadi mtoto atakapotimiza miaka 18 au amepokea diploma ya shule ya upili au sifa ya kimaendeleo ya Kielimu ya Jumla. (GED) sifa.

Wilaya za shule zina sera zote za "udhuru" na "bila udhuru". Wasiliana na wilaya yako ya eneo kwa mahitaji maalum ya eneo lako au ikiwa una maswali kuhusu yasiyokuwemo.

## Je! Ni mahitaji gani ya umri wa kujiandikisha chekechea?

Watoto ambao wana umri wa miaka 5 kufikia au kabla ya Agosti 31 ya mwaka wa shule na ni wakaazi wa Kansas wanastahiki kuhudhuria chekechea katika shule za umma Kansas (sheria ya Kansas KSA 72-3118). Ikiwa ulihamia Kansas kutoka jimbo lingine na mtoto wako alihudhuria chekechea kabla ya kuhamia, basi mtoto wako anastahili kuhudhuria chekechea Kansas.

**KUMBUKA:** If your child completed an accredited kindergarten in another state and, as a result, is ready to attend first grade, your child may still enroll in first grade in Kansas, even if he or she doesn't meet the Kansas age requirement.

Amri za Kansas zinaweza kupatikana mtandaoni kwenye:
http://ksrevisor.org/statutes/ksa_ch72.html

# Je! Ni nyaraka gani zinazohitajika katika kujiandikisha chekechea?

## NYARAKA ZA KUJIANDIKISHA CHEKECHEA:

- Cheti Cha Kuzaliwa

  Ikiwa mtoto wako alizaliwa Kansas, unaweza kupata nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto wako kutoka Idara ya takwimu muhimu ya Kansas kwa barua, barua ya kipaumbele, mtandao, simu, kukutana au faksi. Piga simu 1-877-305-8315, inapatikana masaa 24, siku saba kwa wiki, siku 365 za mwaka. Watafsiri wa kihispania wanapatikana. Chaguo jingine ni kutembelea tovuti yao ya: https://www.kdhe.ks.gov/1186/Birth-Certificate

  **KUMBUKA:** Ikiwa mtoto wako alizaliwa katika jimbo lingine, na hujui ni nani wa kuwasiliana naye ili kupata nakala ya cheti chake cha kuzaliwa, Idara ya Takwimu Muhimu ya Kansas inaweza kukupa taarifa hiyo. Tafadhali wasiliana nao kwa kutumia taarifa iliyo onyeshwa katika aya iliyotangulia.

- Rekodi Ya Kinga (Chanjo)

  Chanjo zifuatazo zinahitajiwa na Sheria ya Kinga ya Kansas ili kuingia shuleni:

  - Mkamba, Pepopunda, Kifaduro (DTap/Tdap)
  - Ugonjwa wa kupooza (IPV/OPV)
  - Ukambi, Matubwitubwi na Rubela
  - Hepatitis A na B
  - Varicella (Tetekuwanga)

  Wanafunzi ambao hawajachanjwa kabisa na ambao hapo awali hawajadai msamaha wa kidini au matibabu wanaweza kutengwa kuhudhuria shule. Kutengwa huku kutakuwepo hadi mtoto atakapomaliza chanjo mfululizo au awasilishe msamaha wa matibabu uliothibitishwa au kusimamishwa (sheria ya Kansas KSA 72-6262).

  **KUMBUKA:** Cheti cha Kansas cha Chanjo kinaorodhesha mahitaji maalum ya kuweka muda wa nafasi ya kati ya vipimo. Hati hii inaweza kupatikana mtandaoni kwa https://www.cdc.gov/vaccines/hcp/imz-schedules/child-adolescent-age.html. Wasiliana na daktari wako au wafanyikazi wa huduma za afya wa wilaya au idara ya afya ya umma ya kaunti kwa mahitaji yaliyoko.




## Tathmini ya Afya ya Kansas (mahitaji ya mwili)

Sheria ya Kansas inahitaji kwamba wanafunzi **WOTE** walio chini ya umri wa miaka 9 ambao wanaingia shule ya Kansas kwa mara ya kwanza lazima watoe matokeo ya tathmini ya afya ya mtoto shuleni ndani ya siku 90 tangu muda wa mwanafunzi kujiandikisha. Tathmini za afya lazima zifanyike ndani ya miezi 12 kabla ya mwanafunzi kuingia shule.

**KUMBUKA:** Mwisho wa kipindi cha siku 90 kinachoruhusu kufuata mahitaji ya tathmini ya afya, wilaya ya shule inaweza kuwatenga wanafunzi kutoka shule, hadi tathmini ya afya ikamilike na matokeo yawasilishwe shuleni. Shule nyingi na jamii hutoa uchunguzi wa bure wa afya wakati wa miezi ya kiangazi. Wasiliana na wilaya yako au idara ya afya ya kaunti kwa taarifa zaidi.

## Fomu Za Idhini

Utaulizwa kusaini fomu za idhini kwa sababu mbali mbali, pamoja na kutoa ruhusa kwa mtoto wako kuhudhuria safari ya nadhalia, kupigwa picha au sababu za kishule kupata rekodi za kimasomo. Shule yako itatoa maelezo kwa kila fomu ya idhini. Kama mzazi au mlezi, utaamua ikiwa unatoa idhini kwa kila ombi.



CHEKECHEA NDANI YA KANSAS

# Mpito wa Chekechea



## **Kujenga Ushirikiano** na Mwalimu wa Mtoto wako:

Kuwa sehemu ya elimu ya mtoto wako huanza wakati wa kuzaliwa na hakukomi kwa sababu ya chekechea! Wajue walimu wa mtoto wako na wafanyikazi wa shule. Fanya mazungumzo ya mara kwa mara yanayohusu kile mtoto wako anafanya, anajifunza, anakiweza na ni wapi anahitaji msaada zaidi. Unaleta taarifa muhimu ambayo inasaidia kuhakikisha mwaka wa chekechea wenye furaha na mafanikio. Sehemu ifuatayo ina vidokezo vya kukusaidia kushiriki kwenye masomo ya mtoto wako.

## **Kusaidia watoto** mpito wa kuingia chekechea:

Kama unavyojua, chekechea ni hatua kubwa. Jitihada za mpito zinapaswa kuanza, ikiwa inawezekana, mwanzo kabla ya mtoto wako kuingia chekechea. Shule nyingi zina siku ya (kutembelea chekechea) ambapo unaweza kumleta mtoto wako kwaajili ya ziara na kujifunza zaidi juu ya shule hiyo.

Malengo ya juhudi zako za mpito lazima yajumuishe:

- Mzoeshe mtoto wako na wewe mwenyewe kwa mwalimu, darasa na shule.
- Toa fursa kwa mwalimu kumjua mtoto wako na kupanga mipango mizuri zaidi kabla ya kuwa mshirika wa darasa.
- Toa fursa za kufahamiana na mwalimu mpya, sera na taratibu za darasa na shule, na pia wanafunzi wenzake wa baadaye na wazazi wao.

Kushiriki katika kutembelea chekechea ni njia rahisi ya kutimiza malengo haya ya mpito, ambayo, pia, husaidia mwalimu wa darasa kuwa tayari kumpokea mtoto wako.

## Taswira Ya Kuingia Chekechea:

### Dodoso la Umri & Hatua ® (**ASQ-3 na ASQ: SE-2**)

Shule za msingi za Kansas zinashirikiana na familia ili kuelewa vizuri maendeleo ya chekechea kwa kutumia Umri & maswali ya hatua®, Toleo la Tatu (ASQ-3), na Maswali ya Hatua: Mihemko ya kijamii, Toleo la Pili (ASQ: SE-2). Maswali haya hutoa picha ya ukuaji wa mtoto. Kwa njia yoyote maswali haya hayatumiwi kuamua ustahiki wa kuingia kwenye chekechea. Kwa kuwa unamjua mtoto wako vizuri zaidi, unakamilisha matoleo yote mawili ya maswali. Kujua zaidi juu ya ustadi na uwezo wa mtoto wako kutakusaidia wewe na walimu wa mtoto wako katika ukuaji na mafanikio ya mtoto wako chekecheani.



Ifuatayo ni orodha ya ujuzi wa kawaida kwa watoto wanaoingia chekechea:

- Hucheza michezo mifupi ya (dakika tano) mwanzo hadi mwisho.
- Anaweza kuvaa koti lake.
- Anazingatia mwelekeo.
- Anatambua namba na rangi.
- Anapenda kusoma, kuimba, kusimulia hadithi na kubadilishana nafasi katika mazungumzo na wengine.

# Viwango Vya Kansas Vya Kujifunza Mapema

## Je! Watoto wanapaswa **kujua nini na kuweza** kufanya nini?

Viwango vya Kansas vya Kujifunza mapema vinaelezea ujuzi na maarifa ambayo watoto wadogo, wenye umri wa kuzaliwa hadi miaka 5, wanapaswa kujua na kuweza kufanya. Ila, maarifa na uwezo hutofautiana sana na watoto hukua kwa viwango tofauti. Mtoto wako anaweza kuwa na ujuzi fulani na sio mwingine na hii ni sawa. Kwa kujua mtoto wako anaweza kufanya nini kunaweza kusaidia kukuza ujuzi mpya.

## Moja ya shughuli bora **ni kusoma**!

Kusoma kila siku husaidia watoto kujifunza maneno, mawazo na shughuli mpya. Kuzungumza na mtoto wako kuhusu picha huwasaidia kujifunza jinsi zinavyohusiana na hadithi. Hivi karibuni, watatunga hadithi zao. Kumsomea mtoto wako pia kutamsaidia kujifunza kusoma kitabu kutoka mbele kwenda nyuma, kushoto kwenda kulia na zaidi. Kuimba, kupiga mayowe, utungo na hadithi zote ni njia muhimu za kufurahisha unapojifunza. Shughuli za kusoma zinazofanyika nyumbani kabla ya chekechea ni kiashiria cha kufaulu kusoma katika shule. Wakati wa kusoma na mtoto wako, onyesha vitu kwenye ukurasa na ujadili kinachotokea; fuata maneno kwenye ukurasa kwa kidole chako unaposoma; na mtoto wako afungue ukurasa. Hizi shughuli zote zinasaidia kusoma. Ushairi ni ujuzi muhimu kwa watoto ambao wanajifunza kusoma. Vitabu vyenye marudio na maneno ya mashairi ni njia nzuri ya kushirikisha Watoto, na zinafurahisha kusoma!

## Watoto hujifunza vizuri kupitia **kucheza**.

Watoto wote wanataka kuchunguza, kujaribu na kufanya wanachokijua na kuelewa. Watoto wanapopata ulimwengu wao kupitia uchezaji, hujifunza kujibu kwa kufikiria na kwa busara kulingana na mazingira yao. Muziki, harakati, mchezo wa kuigiza, michezo na sanaa hufundisha watoto jinsi ya kushiriki wenyewe kwa ubunifu wao wakati wa kukuza uelewa wa kina wa uhusiano kati ya vitu na watu. Kujifunza juu ya ulimwengu wao pia ni pamoja na kushiriki katika familia zao na jamii kupitia mwingiliano wa kijamii. Watoto hujifunza njia za kuishi na matarajio yanaweza kutofautiana kulingana na mazingira (nyumbani dhidi ya gengeni).

Kwa taarifa zaidi, Viwango vya Kansas vya Mafunzo ya Mapema vinapatikana kwenye tovuti ya Idara ya Elimu ya Jimbo la Kansas (KSDE): https://kels.ksde.gov

## **KABLA** Mtoto Wako kuanza Chekechea:




- Shule ya mtoto wako inaweza kukutembelea nyumbani kabla ya chekechea kuanza. Mwalimu anaweza kuwasiliana nawe ili kuweka muda wa kukutana. Ziara za nyumbani humpa mtoto wako nafasi ya kukutana na mwalimu mpya katika mazingira yake mwenyewe. Hii inaweza kupunguza wasiwasi baadaye, kuimarisha hali ya unganisho wa shule na nyumbani na kumpa mwalimu fursa ya kupata hisia ya kibinafsi ya mazingira ya nyumbani ya mtoto wako.
- Muulize mwalimu njia bora ya kupata taarifa kuhusu darasa na shule. Shirikiana na mwalimu katika njia unayopendelea ya mawasiliano.
- Ikiwezekana, panga kutembelea shule hii pamoja na kutumia muda na mwalimu, kuchunguza darasa na kucheza kwenye uwanja wa michezo.
- Shule zingine hutoa kambi za majira ya joto kusaidia watoto kuhamia chekechea. Hakikisha unafuatilia taarifa za programu kama hizo, na kumwandikisha mtoto wako mapema.
- Mruhusu mwalimu ajue masilahi na uwezo wa mtoto wako. Kuwa maalum kutasaidia walimu kujua jinsi ya kushirikiana na mtoto wako katika wiki za kutanguliza.
- Shirikisha wasiwasi wowote au mazingatio maalum kuhusu mtoto wako, kama vile hofu fulani au mzio wa chakula.
- Mwalimu na wafanyikazi wengine wanaweza kutumia tathmini fulani kukusanya taarifa kuhusu ustadi wa mtoto wako, uwezo wake na maarifa. Tathmini ya maarifa ya barua, namba, uelewa wa hadithi na ustadi wa kijamii, itasaidia walimu kuwa tayari kukidhi mahitaji ya mtoto wako - Kumwongozea njia ya mafanikio ya mwaka wa chekechea. Uchunguzi mwingine ni pamoja na kuona na kusikia.
- Ikiwa mtoto wako ameenda shule ya awali, himiza kuwe na mawasiliano kati ya walimu wa chekechea na walimu wa shule ya awali, haswa ikiwa mtoto wako ana mahitaji maalum.
- Wasomee vitabu watoto wako kuhusu kuanza shule (chekechea) na uwe na mazungumzo ya taratibu na mtoto wako ili kumwandaa kwa safari hii ya kufurahisha. Angalia mwisho wa kijitabu ili kupata orodha iliyopendekezwa ya vitabu.
- Unda wiki za kawaida za shule kabla ya shule ili ajifunze kuamka mapema, kujiandaa kwa kitanda na kwenda kulala kwa wakati. Kumbuka kula lishe bora, kufanya mazoezi mengi ya mwili na kulala mara kwa mara ni mambo muhimu katika utaratibu.

## Mara Tu Mtoto **WAKO ANAPO ANZA** Chekechea:



- Watoto wadogo mwanzoni wanaweza kuwa na wasiwasi kwa kutengana au aibu, lakini waalimu wamefundishwa kuwasaidia kuzoea. Kuwa mtulivu na chanya ikiwa mtoto wako analia wakati wa kumuacha. Mhakikishie mtoto wako kuwa atakuwa sawa na kwamba utarudi hivi karibuni. Ikiwa mtoto wako anapata tabu hadi mwezi ukakamilika, kutana na mwalimu na mwanasaikolojia wa shule kukuza mpango wa wakati wa mpito.
- Wakati wa wiki za kwanza za shule, wewe na mwalimu wa mtoto wako mnapaswa kushirikishana taarifa na namna gani nyinyi nyote mnafikiri mtoto wako anarekebishika. Mruhusu mwalimu wa mtoto wako ajue njia bora ya kuwasiliana nawe: kwa simu, maandishi au barua pepe.
- Ikiwezekana, jitolee darasani angalau mara kwa mara katika mwaka. Kufanya hivyo husaidia watoto kuhisi kwamba maisha yao ya shule na familia yanahusiana. Kuwa darasani ni njia nzuri ya kukuza uhusiano na mwalimu wa mtoto wako na wanafunzi wenzake. Utapata pia kujionea mwenyewe mazingira yake ya darasani na ya kawaida. Waalimu wengi wa chekechea wanakaribisha hata msaada wa wazazi wa mara kwa mara, ila hakikisha unauliza kwanza.
- Angalia kila siku vidokezo na vipeperushi kwenye mkoba wa mtoto wako. Hizi ni pamoja na habari muhimu kutoka shuleni.
- Weka muda wa kuzungumza na mtoto wako kuhusu siku yao ya shule, ukiuliza juu ya marafiki wapya, au muhtasari wa siku. Kusikiliza na kutambua hisia na uzoefu wa mtoto wako kutasaidia kujenga ujasiri.

# Kusaidia Kujifunza **KABLA, WAKATI** na **BAADA** ya Chekechea:



- Anzisha ratiba nyumbani na ushikamane nayo. Watoto hufaidika kwa muundo, na hii inaweza kuwasaidia kuzoea ratiba ya chekechea vizuri.
- Fanya kazi na mtoto wako kwa vitu vinavyohusiana na rangi, namba, barua, n.k. kupitia vitabu na michezo. Ni muhimu kufanya mazoea ya kufurahisha na ya kucheza. Walimu wa shule ya awali na chekechea ni rasilimali bora ya mawazo.
- Kutoa uzoefu kwa vitabu, tungo, kuimba, kupaka rangi na kukata, kuzingatia, na kushirikiana na kukaa. Tena, waalimu wa shule ya awali na chekechea wanaweza kutoa maoni ya njia za kufurahisha na za kupendeza za kutoa uzoefu huu.
- Jifunze ratiba ya darasani na ujadili mara kwa mara na mtoto wako. Inapofaa, weka ratiba hizi nyumbani. Kwa mfano, unaweza kumsaidia mtoto wako afanye mazoezi ya kusubiri zamu yake, akiinua mkono wake, akiuliza kwenda bafuni na kumwuliza mwanafunzi mwenzake wacheze.
- Jipange kutumia muda wa utulivu ana kwa ana na mtoto wako wakati wa wiki za kwanza. Weka ratiba ya familia iliyo rahisi kuruhusu marekebisho ya mtoto wako.
- Panga tarehe za kucheza na rafiki mpya (au marafiki) kutoka shule. Kuimarisha uhusiano wa kijamii na wanafunzi wenzake ili kumsaidia mtoto wako kujenga hali ya kujuana na faraja shuleni.
- Tambua tofauti katika ukuaji wa mtoto wako na epuka kulinganisha na ndugu na watoto wengine.
- Punguza muda wa mchezo wa runinga na video na uongeze uzoefu wa vitabu. Tumia wakati wa skrini na taratibu za kujifunza, soma kwa sauti vitabu vya watoto mtandaoni, sanaa, muziki na harakati. Kumbuka wakati mwingi wa skrini hauna afya. Mnamo mwaka wa 2020, Chuo Cha Watoto Cha Marekani (AAP) kiliunda mapendekezo yafuatayo kwenye wakati wa skrini kusaidia familia yako kuamua mustakabadhi unaofaa mtoto wako kutazama yaliyomo kwenye skrini (simu, kompyuta mpakato, kompyuta, runinga):

| Umri wa Mtoto | Saa za Skrini |
|---|---|
| Hadi miezi 18 | Thibiti matumizi ya skrini yawe mazungumzo ya video kwa mwongozo wa mtu mzima. |
| **Watoto wachanga** (miezi 18 hadi miezi 24) | Thibiti kuangalia programu za kielimu na mlezi. |
| **Wanafunzi wa shule ya mapema** (miaka 2 hadi 5) | Thibiti muda wa skrini katika maudhui yasiyo ya kielimu hadi lisaa limoja kwa siku ya wiki na masaa matatu siku za wikendi. |
| **Watoto wenye umri wa miaka** (miaka 6 hadi 10) | Tia moyo tabia nzuri na punguza shughuli ambazo ni pamoja na skrini. |

# Maswali ya nyongeza ambayo unaweza kuwa nayo

| Swali | Jibu / ufuatiliaji |
|---|---|
| Je! Ikiwa nadhani mtoto wangu anahitaji msaada wa ziada? | Ongea kwanza na mwalimu wa chekechea wa mtoto wako ili kupata maoni yake na anavyoelewa mawazo na ustadi wa ujifunzaji wa mtoto wako. |
| Ninajua wapi kuhusu kuzunguka kwa chekechea? | Wapigie simu shule jirani na yako na uulize. Ikiwa hauna uhakika ni shule gani ya mtoto wako, piga simu Kituo cha Usimamizi cha Wilaya. Inapaswa kuwa katika kitabu cha simu au unaweza kuipata mtandaoni hapa: https://www.ksde.gov/Agency/Fiscal-and-Administrative-Services/School-Finance/School-Bus-Safety/Kansas-School-District-Maps. |
| Je! Ikiwa siwezi kumudu vifaa vya shule? | Ongea na mwalimu wa mtoto wako ili kuona ikiwa kuna rasilimali za jamii zinazoweza kusaidia. Kuna jamii nyingi ambazo hutoa vifaa vya shule mwanzoni mwa mwaka wa shule. |
| Siku ya kwanza ya shule ni lini? | Utapata habari nyingi katika kutembelea chekechea. Ikiwa huwezi kuhudhuria, piga simu kwa shule ya mtoto wako na uulize. |
| Je! Nikikosa kutembelea chekechea? Je! Ikiwa tutahamia shule mpya wakati wa majira ya joto? | Watoto wengi hukosa kutembelea. Wasiliana na shule yako uone ikiwa kuna muda wa wewe na mtoto wako kuweza kutembelea shule na kuona darasa lake, kukutana na mkuu wa shule na mwalimu. Hii itakusaidia wewe na mtoto wako kuhisi vizuri kwa mwaka wa chekechea. |
| Vipi kuhusu chakula cha mchana? Je! Mtoto wangu anapata kifungua kinywa? Je! Ikiwa siwezi kununua kifungua kinywa au chakula cha mchana? | Mtoto wako anaweza au asiweze kuwa shule wakati wa chakula cha mchana. Wasiliana na shule kuhusu urefu wa siku ya chekechea. Wanachekechea wa siku nzima watapata fursa ya kula chakula cha mchana shuleni. Shule nyingi kifungua kinywa huwa kinapatikana kwa wanafunzi. Wasiliana na shule ili kujua ikiwa kifungua kinywa kinapatikana. Chakula cha bure na cha bei ya chini kinapatikana kwa familia zinazostahiki. Ikiwa una nia ya kuomba chakula cha bure au cha bei ya chini ya shule, fanya maombi kwa ofisi yako ya shule. |
| Je! Vipi kuhusu programu za kabla na baada ya shule? | Hii inapaswa kuwa habari ambayo hutolewa wakati wa kutembelea chekechea. Unaweza kutembelea tovuti ya wilaya ya shule au kwa kupiga simu katika ofisi ya shule yako kwa taarifa zaidi. |

| Swali | Jibu / ufuatiliaji |
|---|---|
| Ninajifunza wapi kuhusu usafirishaji? | Hii inapaswa kuwa taarifa ambayo hutolewa wakati wa kutembelea chekechea. Unaweza kutembelea tovuti ya wilaya ya shule au kwa kupiga simu katika ofisi ya shule yako kwa taarifa zaidi. |
| Je! Nitaangaliaje rekodi ya mahudhurio ya mtoto wangu, alama / ripoti za maendeleo, kulipia chakula, n.k. | Shule za wilaya hutumia mifumo mbalimbali ili kufuatilia taarifa, mchakato wa malipo ya vitu mbali mbali, kama vile chakula na kuandaa karamu za darasani. Msaidizi wa utawala wa shule anaweza kukusaidia kukufunza juu ya mifumo hii, na pia mwalimu wa mtoto wako. |
| Ninajuaje mtoto wangu yuko salama? | Mawasiliano ni muhimu haswa na mwalimu wa mtoto wako. Muulize mwalimu njia bora ya kuwasiliana naye, wakati wa siku ya shule kwa hivyo ikiwa wasiwasi wa usalama unatokea au unahitaji kuhakikishiwa, unajua jinsi ya kuwasiliana naye. |
| Je! Vifupisho vyote vina maana gani? | Kuna vifupisho vingi vinavyotumika katika elimu. Usisite kuuliza vinavyomaanisha. Hapa kuna mifano michache: |

**EC:** Utoto wa mapema
**ECSE:** Elimu Maalum ya Utoto wa Mapema
**EIS:** Huduma za Kuingilia Mapema
**ELL:** Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza
**ESSA:** Sheria ya Kufanikisha kila Mwanafunzi
**FAQ:** Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara
**FERPA:** Haki za Elimu ya Familia na Sheria ya Faragha
**IDEA:** Sheria ya Elimu kwa Watu walio na Ulemavu
**IEP:** Mpango wa Elimu wa kibinafsi
**KDHE:** Idara ya Afya na Mazingira ya Kansas
**KSDE:** Idara ya Elimu ya Jimbo la Kansas
**LEP:** Uwezo mdogo wa Kiingereza
**MFL:** Elimu kwa Familia ya Wahamiaji
**MTSS:** Mifumo mingi ya Msaada

CHEKECHEA NDANI YA KANSAS

# Orodha ya Kuingia Chekechea

| Mahitaji Ya Mahudhurio Ya Shule Ya Umma | ☒ | Vidokezo |
|---|---|---|
| Mtoto wangu atakuwa na umri wa miaka 5 mnamo au kabla ya Agosti 31. | ☐ | |
| Cheti cha kuzaliwa. | ☐ | |
| Nakala ya tathmini ya afya ndani ya miezi 12 iliyopita (mtihani). | ☐ | Tarehe: |
| Chanjo za mtoto wangu zimesasishwa. | ☐ | |
| Nakala ya chanjo za mtoto wangu. | ☐ | |

| Shule Ya Mtoto Wangu | ☒ | Vidokezo |
|---|---|---|
| Nina nakala, na ninaelewa, sera ya mahudhurio ya shule ya mtoto wangu. | ☐ | |
| Namba ya simu ya shule ya wilaya. | ☐ | Namba: |
| Ninajua ni shule gani mtoto wangu atahudhuria. | ☐ | Jina la Shule:<br>Namba ya simu:<br>Anwani: |
| Nawajua walimu wa mtoto wangu. | ☐ | Jina: |
| Nina orodha ya mahitaji ya kuingia shuleni. | ☐ | |
| Nimejaza fomu ya uandikishaji. | ☐ | |

| Shule Ya Mtoto Wangu | ✗ | Vidokezo |
|---|---|---|
| Nina nakala ya kalenda ya shule na najua muda wa shule kuanza, kukamilika na muda uliopangwa wa mapumziko. | ☐ | |
| Najua saa ambazo mtoto wangu atakuwa shuleni na mahali pa kumchukua. | ☐ | Masaa:<br><br>Wapi: |
| Ninajua kuhusu programu za kabla na baada ya shule. | ☐ | Mawasiliano:<br><br>Wapi: |
| Ninajua kuhusu usafirishaji wa basi. | ☐ | Namba ya basi:<br><br>Wakati wa kukutana na basi: |
| Ninajua kuhusu mpango wa chakula cha mchana. | ☐ | Chakula cha bure na cha bei ya chini kinapatikana kwa familia zinazostahiki. Ikiwa una nia ya kuomba chakula cha bure au cha bei ya chini shuleni, fanya maombi kwenye ofisi yako ya shule. |
| Ninajua kuhusu kutembelea shule ya chekechea. | ☐ | Tarehe:<br><br>Wakati: |
| Nimekamilisha fomu ili mtu mwingine aweze kumchukua mtoto wangu ikiwa kuna dharura. | ☐ | Mtu:<br><br>Taarifa ya dharura: |
| Ninajua kuhusu PTA / PTO au shirika lingine la wazazi shuleni. | ☐ | Mawasiliano:<br><br>Nyakati za mkutano: |
| Nimepokea nakala ya kitabu cha shule. | ☐ | |

# Rasilimali

## Vitabu:

"Countdown to Kindergarten" na Alison McGhee

"Mrs. Bindergarten Gets Ready for Kindergarten" na Joseph Slate na Ashley Wolff

"The Night Before Kindergarten" na Natasha Wing na Julie Durrell

"Look Out Kindergarten, Here I Come!" na Nancy Carlson

"Welcome to Kindergarten" na Anne Rockwell

## Rasilimali za mtandaoni:

Kituo Cha Rasilimali Ya Habari Ya Mzazi Kansas:
www.ksdetasn.org/kpirc

Idara Ya Elimu Ya Jimbo La Kansas:
www.ksde.gov

Chama Cha Kitaifa Cha Elimu Ya Watoto Wadogo:
www.naeyc.org

Viwango Vya Kitaifa vya PTA Ushirikiano Wa Familia Shuleni:
www.pta.org/nationalstandards

1-800-Ushirikiano Wa Watoto Na Wazazi umewezeshwa na Jumuiya Ya Huduma Ya Watoto Kansas:
www.1800childrenks.org



For more information, contact:

KSDE Early Childhood
(785) 296-6602
Amanda.Petersen@ksde.gov

Kansas State Department of Education
900 S.W. Jackson Street, Suite 102
Topeka, Kansas 66612-1212

www.ksde.gov